IDARA YA LUGHA
APRILI MWAKA 2020
KIDATO CHA NNE
102/1 – KISWAHILI – Karatasi ya 1
INSHA
Jina ___Nambari Ya Usajili ___Dar__
Maagizo
(a) Andika insha ZOTE.
(b) Kila insha isipungue maneno 400.
(c) Kila insha ina alama 20.
(d) Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

1. Andika wasifu wa kiongozi umpendaye.
2. Uavyaji wa mimba una madhara mengi mno. Jadili.
3. Andika insha kuhusu methali "mgagaa na upya hali wali mkavu"
4. Malizia insha kwa maneno ...watoto wangu ni vyema kuwatii na kuwaheshimu wazazi wenu. Mjue kuwa asiyeskia la mkuu huvunjika guu.

IDARA YA LUGHA
APRILI MWAKA 2020
KIDATO CHA NNE

102/3 – KISWAHILI – Karatasi ya 3
FASIHI

Maagizo:

a) Jibu maswali YOTE katika Karatasi hii.
b) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
SEHEMU A: HADITHI FUPI
TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE (DUMU KAYANDA NA ALIFA CHOKOCHO)
1. Hadithi ya Kidege (Robert W. Oduori) imejengwa kwenye jazanda. Eleza hali hii kwa kutolea hoja ishirini. ( alama 20)

SEHEMU B: RIWAYA
CHOZI LA HERI (ASSUMPTA K. MATEI)
2. " Unyonge haukuumbiwa majimbi, ulitunukiwa makoo ..."
a) Eleza muktadha wa dondoo. ( alama 4)
b) Tolea sifa nane za msemezwa. ( alama 8)
c) Jadili suala la ubabedume na athari zake katika riwaya. ( alama 8)
3. Watoto katika jamii hukumbwa na changamoto nyingi sana. Jadili kauli hii kwa kutolea hoja ishirini. ( alama 20)

SEHEMU C: TAMTHILIA
KIGOGO (PAULINE KEA)
4. “muhimu ni kuwa mimi kura yangu simpi mtu mwingine…”
a) Eleza muktadha wa dondoo. ( alama 4)
b) Tambua sifa sita za msemaji. ( alama 6)
c) Linganisha mhusika Majoka na mhusika Kenga. ( alama 10)

5. Jadili maudhui yafuatayo katika tamthilia:
i) Umaskini
ii) Ndoa na mapenzi
iii) Elimu ( alama 20)

SEHEMU D: USHAIRI
6. Shairi A
Eti
Mimi niondoke hapa
Niondoke hapa kwangu
Nimesaki, licha ya risasi
Vitisho na mauaji, siondoki

Mimi
Siondoki
Siondoki siondoki
Niondoke hapa kwangu!
Kwa mateke hata na mikuki
Marungu na bunduki, siondoki

Hapa
Siondoki
Mimi ni Pahame!
Niondoke hapa kwangu!
Fujo na ghasia zikizuka
Na kani ya waporaji, siondoki

Haki
Siondoki
Kwangu siondoki
Niondoke hapa kwangu!
Nawaje; waje wanaokuja
Mabepari wadhalimu, siondoki

Kamwe
Siondoki

Ng’oo hapa kwangu!
Katizame chini mti ule!
Walizikwa babu zangu, siondoki

Sendi
Nende wapi?
Si hapa kitovu changu
Niondoke hapa kwangu
Wangawa na vijikaratasi
Si kwamba hapa si kwangu, siondoki

Katu
Siondoki
Sihitaji karatasi
Niondoke hapa kwangu
Yangu mimi ni ardhi hii
Wala si makaratasi, siondoki

Maswali

a) Shairi hili ni la aina gani? Kwa nini (alama 2)

b) Taja masaibu anayopitia mzungumzaji (alama 4)

c) Eleza toni ya shairi hili (alama 2)

d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 3)

e) Tambua matumizi ya mbinu ya usambamba (alama 2)

f) Andika ubeti wa tano kwa lugha nathari (alama 4)
g) Tambua idhini moja ya mtunzi (alama 1)
h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi (alama 3)
(i) Karatasi
(ii) Nimesaki
(iii)kitovu

7. Shairi B
Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.
Nilipokuwa nimekanyaga, kidato cha kwanza, nikipanda ngazi,
Nyuma nderemo zimechaga, watu wanacheza, wote wamenenzi
Nikatua kuvua maninga, nikayakaza, upeo wa ngazi,
Mbaali nikauona mwanga, halafu, kiza, mwanga kikienzi,
Niliogopa.

Nako nyuma nilipotizama, nilikotoka, nilikozalika,
Babangu ali amesimama, jembe ‘meshika, amesawijika,
Kando mama amenitazama, chozi latoka, kajawa wahaka,
Tafakuri zao zimezama, wamelimbuka, nilinyereka,
Nilitishika.

Wote tuli tumetazamana, macho metuna, yakisemezana,
Midomo ilitaka kunena, ikaubana, kauli hakuna,
Hisi, imani, vikapigana, moyo ‘mebana, kichwa kimetuna,
Busara nzuri ikanikana, kinywa kunena, kutoa hiyana,
Nilisikitika.

Mara macho yalinifunguka, upya kuwaona, damu lichemka,
Kaki la baba liloraruka, ndio dhamana, si haba miyaka,
Rindale mama limekongoka, rangi halina, bali lavalika,
Ujasiri wangu uling’oka, ‘n’ kawaza jana, nilivyoleleka,
Niliathirika.

Huko mbele ninako angaza, si pa amani, wala tumaini,
Hata nao kuliwashangaza, nakuende’ni, kuzama gizani?
Niwaache wakila majaza, mbe’ hawaoni, yao afueni,
Nilisita nikajiuliza, nini thamani, kufia jirani?
Nilijisaili.

Pendo na amani lilinivaa, n’kawarudia, kwikwi limenikaba,
Japo kauli ‘linikataa, niliwaapia, jukumu kubeba,
Nikawaomba yao ridhaa, nyuta kutwaa, madhambi kubeba,
Minderemo ilishangilia, ngoma kulia, ikanipa hiba,
Sikutamauka.

Maswali.

a. Taja na ueleze bahari mbili zinazodhihirika kwa mujibu wa mishororo.(alama 2)
b. Eleza sifa za kiarudhi zinazodhihirika katika ubeti wa pili.(alama 4)
c. Fafanua sababu ya furaha inayojitokeza katika ubeti wa kwanza na wa mwisho. (alama 4)
d. Mshairi anadai kutishika, kusitikisha na kuathirika. Fafanua kulingana na shairi hili. (alama 3)
e. Andika ubeti wa nne katika lugha ya nathari. (alama 4)
f. Toa miundoo miwili ya mifano ya maneno ya inkisari iliyotumika katika shairi hili. (alama 2)
g. Urejeshi umetumika kwa jinsi gani katika ubeti wanne. (alama 1)

8. SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI
a) Eleza maana ya ngano. ( alama 2)
b) Tambua sifa sita za masimulizi. ( alama 6)
c) Je, formula ya ufunguzi huwa na umuhimu upi katika kuwasilisha hadithi? ( alama 5)
d) Fafanua sifa za mtambaji bora za hadithi. ( alama 7)

IDARA YA LUGHA
APRILI MWAKA 2020
KIDATO CHA NNE

102/3 – KISWAHILI – Karatasi ya 3
FASIHI

Maagizo:

c) Jibu maswali YOTE katika Karatasi hii.
d) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

Nalitazama jua likichwa,
Matumaini yangu yakizama pamoja
na miale miekundu
Nalidhani lilikuwa jinamizi tu
Kwamba ulikuwa kesha n'acha
Walikuwa wameisha n'ambia
Walimwengu
Ela nilikataa katakata walosema
Nikajitia kuamini waloamba yalikuwa
Uzushi
Hadi siku hii nilopokea waraka,
Waraka ambao ulikuwajeneza ka kuzikia
Pendo letu la miongo miwili.

a) Huu ni wimbo wa aina gani? ( alama 2)
b) Fafanua sifa nane za nyimbo hizi. ( alama 8)
c) Je, nyimbo hizi zina dhima gani katika jamii. ( alama 8)
d) Tambua toni ya wimbo huu. Tolea sababu. ( alama 2)

SEHEMU B: TAMTHILIA YA KIGOGO (Pauline Kea)

2. " Uliona nini kwa huyo zebe wako? Eti mapenzi!"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. ( alama 4)
b) Fafanua mbinu mbili za lugha katika dondoo. ( alama 4)
c) Je, ni sifa gani za msemaji zinazodhihirika katika dondoo? ( alama 2)
d) Jadili suala la mauti katika tamthilia nzima. ( alama 10)

3. (a) Fafanua jinsi mwandishi wa Kigogo alivyofanikisha matumizi ya Majazi.
( alama 10)

(b) Utawala wa mbaya ni tatizo sugu katika mataifa mengi barani Afrika. Tetea kauli hii kwa kutolea hoja kumi kutoka kwenye tamthilia. ( alama 10)

SEHEMU C: RIWAYA YA CHOZI LA HERI (Assumpta K. Matei)

4. “Umewahi kumwona mtoto wa miaka hamsini ambaye hajasota; sikwambii kusimama dede?”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. ( alama 4)
b) Tambua mbinu mbili za lugha katika dondoo. ( alama 4)
c) Eleza sifa nne na mnenaji. ( alama 4)
d) Jadili kikamilifu hasara za ukabila kwa mujibu wa Riwaya nzima.( alama 8)

5. Mwanamke ni kiumbe mwenye changamoto si haba. Tetea kauli hii kwa kutolea hoja ishirini kutoka kwenye Riwaya. ( alama 20)

SEHEMU D: HADITHI FUPI YA TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE ( Dumu Kayanda Na Alifa Chokocho)

Mtihani Wa Maisha ( Eunice Kimaliro)

6. “ Sikuzaa mwana, nilitoa tu maradhi tumboni”
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. ( alama 4)
b) Bainisha mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondoo. ( alama 2)
c) Ni kipi kilichomfanya msemaji kuyasema hayo ? ( alama 4)
d) Fafanua sifa tano za msemezwa. ( alama 5)
e) Jadili maudhui ya elimu katika hadithi hii. ( alama 5)

7. Jadili maudhui ya umaskini katika hadithi zifuatazo: ( Alama 20)
a) Tumbo Lisiloshiba
b) Mapenzi ya Kifaurongo
c) Ndoto ya Mashaka
d) Nizikeni Papa Hapa
e) Mwalimu Mstaafu

SEHEMU E: USHAIRI

SHAIRI 1
Ya wapi silika hino, ya kwenda kinyumenyume?
Nilijibu hata kwa wino, majibuyo niyasome,
Kuno ‘geuza maneno, na kuyafanya maleme,
Haramu kuwa halali, insani twajilaani.

Insiya jilaani, ni bora wazi niseme,
Kukubalia idhini, mimba wakazikateme,
Hiyo nayo haki gani, wasiyoona mit ume,
Haramu kuwa halali, insani twajilaani.

Twajilaani laana, kijitakia ujume,
Nayo habari hatuna, twajiletea ukame,
Pia habari hatuna, ni wana sio vimeme,
Haramu kuwa halali, insani twajilaani.

Muswada siyo halali, wakuviavya vikembe,
Utawapea halali, mabinti wetu watambe,
Magulamu ja fahali, nao wakame pembe,
Haramu kuwa halali, insani twajilani.

Kuavya mimba ni dhambi, ya kumuudhi Rahimu,
Laana twajaza tumbi, ya moto wa jahanamu,
Tuache vino vitimbi,turudie utimamu,
Haramu kuwa halali, insani twajilani.

Jambo hili nawambia, litazidisha ukware,
Ni ya uvundo tabia, ni afueni tuisare,
Tuweze kuitubia, tuwache zino parare,
Haramu kuwa halali, insani twajilani.

Muida ndio sinao, nina mengi ya kusema,
Wapigania hakio, zingatia nayosema,
‘sipashe mswada huo , ni madhambi ya kuchoma,
Haramu kuwa halali insani twajilani.

MASWALI
a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili . (alama 1)
b) Eleza muundo wa shairi hili . (alama 4)
c) Kwa kutolea maelezo mwafaka,tambua bahari tatu katika shairi hili . (alama 3)
d) Eleza tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika shairi na utolee ithibati (alama 2)
e) Onyesha jinsi idhini ya mtunzi ilivyotumika kutimiza arudhi katika shairi hili. (alama 4)
f) Bainisha toni ya shairi hili . (alama 1)

g) Tambua maudhui mawili yanayotawala shairi hili . (alama 2)
h) Tambua madhara matatu ya uavyaji mimba . ( alama 3)
SHAIRI 2
1. Kama wanipenda kweli „sinipe katu pilau
Kama wanipenda kweli „sinipe hata na pau
Kama wanipenda kweli nipe chakula cha wenzi
Kama wanipenda kweli!

2. Kama wanipenda kweli usinipe vazi kuu
Kama wanipenda kweli „sinipe pambo la juu
Kama wanipenda kweli nivishe vazi la wenzi
Kama wanipenda kweli!

3. Kama wanipenda kweli „sinifanye wako nyuni
Kama wanipenda kweli „sinifungie tunduni
Kama wanipenda kweli niache niruke huru
Kama wanipenda kweli!

4. Kama wanipenda kweli „sinifanye asumini
Kama wanipenda kweli „sinimee kitaluni
Kama wanipenda kweli n‟ache ninawiri huru
Kama wanipenda kweli!

5. Kama kweli wanipenda „sinite mimi ratabu
Kama kweli wanipenda „sinishabihi zabibu
Kama kweli wanipenda niite mtu kwa dhati
Kama kweli wanipenda!

6. Kama kweli wanipenda „sinite paa muhibu
Kama kweli wanipenda „sinizonge kwa nasabu
Kama kweli wanipenda „sikiza yangu sauti
Kama kweli wanipenda!

7. Kama kweli wanipenda nikuonye matendano
Kama kweli wanipenda na tueke mapatano
Kama kweli wanipenda nitende na we‟ utende
Kama kweli wanipenda!

8. Kama kweli wanipenda tuufungue wiano
Kama kweli wanipenda yawepo masikizano
Kama kweli wanipenda utende na mi‟ nitende
Kama kweli wanipenda!

9. Kama wanipenda kweli subu nyama za ulimi
Kama wanipenda kweli zigo „sinitwishe mimi
Kama wanipenda kweli niepushie utemi
Kama wanipenda kweli!

MASWALI

a. Lipe shairi hili anwani mwafaka . (alama 1)
b. Eleza aina ya shairi hili. (alama 1)
c. Taja na ufafanue tamathali moja ya usemi liyotawala katika shairi hili. (alama 2)
d. Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
e. Eleza bahari ya shairi hili. (alama 3)
f. Andika ubeti wa nne kwa lugha tutumbi. (alama 4)
g. Fafanua Uhuru wa mshairi. (alama 2)
h. Andika maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (alama 2)
a) Kitaluni
b) Muhibu

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOCHAPISHWA.

IDARA YA LUGHA
APRILI MWAKA 2020
KIDATO CHA NNE
102/2 – KISWAHILI – Karatasi ya 2
JINA__________________________________________ DAR_______

1. UFAHAMU: (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia.

Mawasiliano ni upashanaji habari kwa namna tofautitofauti. Njia za mawasiliano zimebadilika sana katika historia ya binadamu. Kwa mfano, zamani ingechukua siku nyingi kupitisha ujumbe baina ya watu wanaoishi sehemu mbalimbali. Siku hizi ujumbe hupitishwa katika sekunde chache katika masafa marefu.

Ugunduzi wa simu uliofanywa na Alexander Graham Bell mwaka wa 1876 ulifungua ukurasa mpia katika mawasiliano. Nchini Kenya, miaka ya sabini na themanini, ilikuwa vigumu kupata huduma za simu. Mtu alihitajika kusafiri masafa marefu ili kupata huduma hizo hasa kwa wale walioishi mashambani. Aidha kutokana na ukosefu wa huduma hizo katika sehemu nyingi, mtu alihitaji kupiga foleni ili ahudumiwe ama ajihudumie.

Baadaye, simu tamba zilivumbuliwa na mawasiliano yakarahisisishwa. Mwanzoni, simu tamba zilikuwa vidude vikubwa ambavyo havikutoshea mifukoni. Hata hivyo, usumbufu huo ulitafutiwa suluhu. Siku hizi simu tamba ni ndogo na hivyo huwa rahisi kuzibeba. Aidha, kampuni za kutoa huduma za mawasiliano na kufanya gharama ya kupiga simu kuenda chini.

Barua pia ni njia ya mawasiliano na imetumika kwa muda mrefu. Baadhi ya nchi kuliko

tumiwa barua katika enzi za zamani ni Misri na Uyunani. Matarishi walitumwa kupeleka barua. Barua zilichukua muda mrefu kufikia aliyeandikiwa. Aidha kutokana na kwamba si watu wote waliojua kusoma na kuandika, wachache waliokuwa na maarifa hayo waliwandikia na kuwasomea. Katika enzi hizi matumizi ya barua yamepunguzwa kwa kiwango kikubwa na tarakilishi na simu tamba. Kwa kutumia tarakilishi unaweza kutuma barua pepe. Aidha, kwa kutumia simu tamba unaweza kutuma arafa.

Waajiri wengi hupendekeza wanaoomba kazi watume maombi yao kwa kutumia baruapepe. Njia hii huondoa uwezekano wa wanaoomba kazi kutumia ufisadi ili wapate kazi. Aidha, njia hii husaidia kutunza mazingira kwani karatasi hazitumiwi.

Katika elimu tarakilishi zinatumiwa shuleni kufundishia hivyo kurahisisha mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Aidha, kupitia tarakilishi iliyotandawizwa ama kuunganishwa kwa mtandao, watu huweza kujuliana hali na kupashania habari mbalimbali kutoka pembe zote za dunia. Changamoto katika hatua hii ni ukosefu wa nguvu za umeme hasa mashambani. Aidha,gharama ya kununua tarakilishi ni kali mno hasa kwa mataifa yanayoendelea ikizingatiwa kuwa yana changamoto za kimsingi kama vile kutojua kusoma na kuandika, magonjwa na umaskini.

Vilevile, redio ni chombo muhimu ambacho huchangia sana katika mawasiliano. Kwa sasa, hiki ndicho chombo cha pekee kinachomilikiwa na karibu kila familia. Hali hii inachangiwa na ukweli kwamba kunazo redio ndogo ambazo hutumia betri. Chombo hiki huwapitishia matangazo na habari kuhusu yanayotendeka kutoka pande zote za ulimwengu. Redio hufahamisha, huburudisha na kuelimisha. Wizara ya Elimu imekuwa ikitumia redio kufundishia masomo mbalimbali hasa katika shule za msingi.

Nani asiyejua kuhusu runinga? Chombo hiki pia hutoa mchango mkubwa katika mawasiliano. Runinga hushirikisha hisi za kusikiliza na kuona, kwa hivyo mawasiliano yake hufanikiwa sana. Hata hivyo, ni asilimia ndogo ya watu ambao wanaweza kuimiliki kutokana na gharama yake na pia si wengi wanazo nguvu za umeme majumbani mwao.

Mwalimu ni muhimu sana katika maendeleo ya jamii oyote. Ni dhahiri shahiri mwasiliano ni sehemu muhimu katika kuimarika kwa uchumi. Vile vile huwezesha watu kutangamana na kubadilishana mawazo. Binadamu si kama visiwa vinavyosimama peke yavyo. Binadamu huhitaji kutangamana na binadamu wengine katika maisha na kwa hivyo mawasiliano ni muhimu.

a) Eleza kini cha taarifa hii. (al. 1)

b) Toa sababu mbili za waajiri kuhimizi matumizi ya barua pepe. (al. 2)

---

c) Kwa nini redio ndicho chombo kinachotegemewa zaidi katika mawasiliano. Eleza sababu nne. (al. 4)

d) Kwa mujibu wa kifungu hiki eleza udhaifu wa tarakilishi. (al. 3)

e) Eleza faida mbili za tarakilishi. (al. 2)

---

f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa. (al. 2)
i) Kupiga foleni ¬¬¬¬¬¬¬¬¬¬¬¬¬ ¬

ii) Matarishi

2. UFUPISHO: (ALAMA 15)
Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali yafuatayo
Lugha ndio msingi wa maandishi yote. Bila lugha hakuna maandishi. Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha husitawisha ufahamu wetu wa mambo tusomayo. Mazoezi katika kuandika husitawisha ufahamu katika kusoma kwa sababu katika kuandika ni lazima kuyatumia maneno vizuri na kufahamu ugumu wa usemi. Twajifunza matumizi ya lugha katika kuzungumza na kuwasikiliza wengine wakizungumza. Lugha tusomayo ni anina ya lugha ya masungumzo.
Kuna ujuzi mwingi katika kuzungumza kama vila michezo ya kuigiza, hotuba, majadiliano na mazungumzo katika darasa. Haya yote husaidia katika uhodari wa matumizi ya lugha. Ujuzi wa kila siku utasaidia katika maendeleo ya kusoma na usitawi wa msamiati. Ikiwa mwanafunzi amemwona ndovu hasa, atakuwa amejua maana ya neno ndovu vizuri zaidi kuliko mwanafunzi ambaye hajawahi kumwona ndovu bali ameelezwa tu vile ilivyo. Vilevile ujuzi wa kujionea sinema au michoro husaidia sana katika yaliyoandikwa. Ikiwa mwanafunzi ana huzuni au ana furaha, akiwa mgonjwa au amechoka au amefiwa, haya yote ni ujuzi. Wakati juao mwanafunzi asomapo juu ya mtu ambae amepatikana na mambo kama huyo hana budi kufahamu zaidi.
Karibu elimu yote ulimwenguni huwa imeandikwa vitabuni. Hata hivyo, lugha zote hazina usitawi sawa kuhusu fasihi. Kwa bahati mbaya lugha nyingine hazijastawi sana na hazina vitabu vingi. Fauka ya hayo , karibu mambo yote yanayohusiana na elimu huweza kupatikana katika vitabu kwenye lugha nyingine.
Inambidi mwanafunzi asome vitabu au majarida juu ya sayansi au siasa au historia, lakini haimbidi kusoma tu juu ya taaluma fulani anayojifunza . Inafaa asome juu ya michezo, mambo ya mashairi na juu ya mahali mbalimbali ili kupata ujuzi wa mambo mengi.
a) Fupisha aya za kwanza mbili kwa kutumia maneno 65 (alama 10, 1 ya utiririko)
Matayarisho

Jibu

b) Kwa kuzingatia habari zote muhimu na bila kupoteza maana asilia, fupisha aya ya mwisho
(Maneno 30) (alama 5 utiririko)
Matayarisho

Jibu

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)
a) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya vielezi viwili vya silabi moja. (al. 2)
b i) Eleza maana ya sauti za likwidi. (al. 1)
ii) Toa mifano ya sauti za likwidi. (al. 1)
c) Ainisha mofimu: Lililoliwa (al. 3)

d) Eleza huku ukitoa mifano matumizi mawili ya kiambishi 'ji'. (al. 2)
e) Huku ukionyesha upatanisho wa kisarufi katika sentensi, weka nomino zifuatazo katika ngeli mwafaka. (al. 2)
i) Uwele

ii) Vita

f) Tumia 'O' rejeshi tamati kuunganisha sentensi zifuatazo. (al. 1)
Tawi limekauka
Tawi limeanguka
g) Tambua vivumishi na uonyeshe ni vya aina gani. (al. 3)
Wanafunzi wawa hawa waliochelewa watafanya kazi ya sulubu kama adhabu.
h) Kanusha: Msichana ambaye amefika ametuzwa. (al. 1)
i) Onyesha aina za virai katika sentensi hii: (al. 2)
Wale wazazi wetu watawasili kesho saa tatu.
j) Unda nomino kutokana na kitenzi 'Haribu' (al. 1)

k) Tambua aina za vitenzi katika sentensi. (al. 2)
Hawa sio wachezaji bali wamekuwa wakichezea timu hii.

l) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya viunganishi vya kulinganua. (al. 1)
m) Eleza matumizi mawili ya 'ka' . Toa mifano katika sentensi. (al. 2)

n) Andika visawe ya maneno yafuatayo (al. 2)
i) Daawa
ii) Ainisha
o) Onyesha kwa kauli ulizopewa (al. 1)
i) Ja (tendewa)
p) Andika kinyume: Tajiri aliyesifiwa amelaaniwa. (al. 1)
q) Changanua sentensi hii kwa kutumia vishale. (al. 4)
Yule mgeni aliyefika jana ameondoka leo.

r) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo (al. 2)
Oyula atapendwa na wengi ikiwa atashinda leo.
s) Eleza majukumu mawili ya chagizo huku ukitoa mifano. (al. 2)
t) Akifisha. (al. 3)
sikiliza bwana mdogo siku hizi tunaishi katika jamii ambayo imebadilika hayo mawazo

yako ya zama kongwe hayatakufikisha popote kumbuka u) Andika ukubwa wa sentensi katika wingi. Nyundo imo ndani ya kibweta. (al. 1)

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

a) Eleza matatizo matano yanayowakabili wazungumzaji wa Kiswahili. (al. 10)

IDARA YA LUGHA
APRILI MWAKA 2020
KIDATO CHA NNE
102/1 – KISWAHILI – Karatasi ya 1
INSHA

Jina ________________________________Nambari Ya Usajili _______Dar_____

Maagizo

(e) Andika insha ZOTE.
(f) Kila insha isipungue maneno 400.
(g) Kila insha ina alama 20.
(h) Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

1. Wewe ni katibu wa tume ya kuchunguza chanzo cha ajali barabarani. Andika ripoti.
2. Ugonjwa wa Corona una hasara nyingi kuliko faida. Jadili.
3. Andika kisa kitakachoafiki methali “ kifo cha nyani kifikapo miti yote huteleza.”
4. Andika insha itakayokamilika kwa maneno haya. Nilimwangalia mama yangu mzazi usoni na kumshukuru sana kwa kunilea na kunipa elimu bora iliyonisaidia sana maishani.

IDARA YA LUGHA
APRILI MWAKA 2020
KIDATO CHA NNE
102/2 – KISWAHILI – Karatasi ya 2

JINA_____________________________________ DAR______

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Tofautisha sauti zifuatazo. ( alama 3)

i. /l/ na /r/ ______

ii. /f/ na /v/______

iii. /s/ na /z/ _____

b) Unda neno lenye muundo huu. KI-KKKI ( alama 1)

c) Tofautisha silabi wazi na silabi funge. ( alama 1)

d) Tofautisha baina ya ala tuli na ala sogezi na utolee mifano. ( alama 2)
e) Weka kiimbo katika sentensi hii ili kuleta dhana tatu tofauti. ( alama 3 ) Juma ni mwizi

f) Maneno haya yako katika ngeli zipi ? ( alama 2)

i. Nyua ____

ii. Kifaru ___

g) Tunga sentensi moja ili kudhihirisha hali isiyodhihirika. ( alama 1)

______________
h) Bainisha viambishi katika neno hili: ( alama 3)
Alipomlilia

i) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. ( alama 3)
Nomino+ Kishazi Tegemezi+Kitenzi+Kihusishi+Nomino

_______
j) Tolea maana mbili za sentensi hii. ( alama 2)
Hosea alimwona Maria akiwa kanisani

_______

k) Tumia ni ili kuibua maana tatu kisarufi. ( alama 3)

_______
l) Nyambua vitenzi hivi katika kauli ya kutendesha. ( alama 2)

i. Lewa ___

ii. Nya ___
m) Changanua sentensi hii kwa njia ya masanduku. ( alama 4)
Ingawa alisoma kwa bidii hakupita mtihani wake.

n) Bainisha aina za maneno katika sentensi. ( alama 3)
Mtoto wa mwalimu alikuwa akiwapiga sana

o) Tambua virai katika sentensi. ( alama 2)
Wazee wale watakuwa mjini kesho.

_______
p) Tambua vishazi katika sentensi hii.
Angesoma kwa bidi angepita mtihani huo.

___________
q) Eleza maana ya misemo hii. ( alama 2)

i. kula kalenda __________

ii. vaa miwani ________

r) Mtu aliye na shida fulani ndiye hufahamu vyema uzito ulioko. Je, ni methali gani inaafiki hali hii? ( alama 1)

_____________

s) Eleza maana ya kijalizo. ( alama 1) _____

_______

ISIMUJAMII (ALAMA 10)

a) Jadili madai kuwa Kiswahili ni lugha ya kibantu. ( alama 5)

________________

b) Eleza hoja tano kuhusu sifa za lugha ya taifa. ( alama 5)

_____________

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOCHAPISHWA

Kiswahili Kidato Cha Tatu
Maswali Ya Tamthilia Ya Kigogo (Pauline Kea) Alhamisi 02.04.2020
Tanbihi: Fasihi ni mifano. Kila jawabu lazima liwe na hoja kuu, maelezo na kisha mfano mwafaka.
SWALI 1
“Nimekuja kuwakomboa”
(a)Eleza muktadha wa dondoo hili (alama
(b)Kwa kutumia hoja kumi na mbili,thibitisha kuwa msemewa na wenzake walistahili kukombolewa (alama12)
(c)Kwa kutumia hoja nne eleza umuhimu wa msemewa (alama4)

SWALI 2
Tamthilia ya kigogo ni kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za kiafrika.Thibitisha (alama20)

SWALI 3
Onyesha namna mwandishi alivyofanikiwa kukuza maudhui yafuatayo:
(i) Elimu (alama10)
(ii)Ujana (alama10)
SWALI 4
Mvunja nchi ni mwananchi ‘Eleza ukweli wa kauli hii kwa kurejelea matukio katika tamthlia ya kigogo. (alama20)

SWALI 5
“Uliona nini kwa huyo Zebu wako? Eti mapenzi!
a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama4)
b)Andika mbinu mbili za lugha zinazojitokeza kwenye dondoo hili. (alama4)

c)Taja hulka nne za msemaji. (alama4)
d)Fafanua umuhimu wa msemaji katika tamthilia ya kigogo. (alama8)

SWALI 6
Masaibu ya wanasagamoyo ni sawa na yale yanayoyakumba mataifa mengi katika bara la Afrika. Thibitisha kwa kutoa mifano ishirini. (alama20)

SWALI 7
Kwa kurejelea tamthilia ya 'Kigogo Ya Pauline Kea,onyesha jinsi ambavyo viongozi wengi katika nchi za kiafrika wamejawa nal tamaa.

IDARA YA LUGHA
APRILI MWAKA 2020
KIDATO CHA NNE

102/3 – KISWAHILI – Karatasi ya 3
FASIHI

Maagizo:

e) Jibu maswali YOTE katika Karatasi hii.
f) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

SEHEMU A- RIWAYA: CHOZI LA HERI (ASSUMPTA K. MATEI)

1. " unatumia mantiki gani kusema kuwa sisi si watoto wa miaka hamsini?"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. ( alama 4)
b) Tambua mbinu mbili za lugha katika dondoo hili. ( alama 4)
c) Eleza kwa kina maafa yaliyompata msemezwa wa dondoo hili. ( alama 8)
d) Tambua kisha ueleze sifa nne za msemaji. ( alama 4)

SEHEMU B- TAMTHILIA: KIGOGO (PAULINE KEA)
2. " Sipendi hii mitandao ya kijamii…"
a) Eleza muktadha wa dondoo. ( alama 4)
b) Fafanua sifa nane za msemaji. ( alama 8)
c) Je, vyombo vya habari vilikuwa na mchango upi katika ukombozi wa Sagamoyo? ( alama 8)

3. Majoka ni joka. Jadili kauli hii kwa kutolea hoja ishirini na mifano mwafaka. ( alama 20)

SEHEMU C- HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE (DUMU KAYANDA NA ALIFA CHOKOCHO)
Tumbo Lisiloshiba (Said A. Mohammed)

4. “ Sheria gani imo mikononi mwetu?”
a) Eleza muktadha wa dondoo. ( alama 4)
b) Fafanua sifa sita za msemaji. ( alama 6)
c) Mwandishi wa hadithi hii amefanikisha matumizi ya jazanda. Jadili ( alama 10)

5. Jadili mashaka ya Mhusika Mashaka katika hadithi ya Ndoto ya Mashaka (Ali Abdulla Ali)

6. USHAIRI
Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali.
Mungu naomba subira, subira nayo imani
Imani iliyo bora, bora hapa duniani
Duniani mwa kombora, kombora nayo hiani
Hiani pamwe ukora wenye kuhini.

Kuhini kwenye kiburi, kiburi na ufidhuli
Ufidhuli wa kudhuri, kudhuri wangu muwili
Muwili hata kidari, kidari kuwa thakili
Thakili kisinawiri, kisinawiri misuli.

Misuli kuwa hafifu, hafifu kama muwele
Muwele wa hitilafu, hitilafu ya nduwele
Nduwele kutakilifu, kutakilifu milele
Milele kutoniafu, kutoniafu na vishale.

Vishale vinitomele, vinitomele vikwato
Vikwato pia maole, maole kufanya mito
Mito ya matozi tele, tele mithili kitoto
Kitoto kilo vipele, vipele vyenye fiakuto.

Fukuto lanipa neno, neno hili kutamka
Kutamka wazi vino, vino subira kutaka
Kutaka imani mno, mno n’sipate wahaka
Wahaka wa matukano, matukano na mashaka.

Mashaka haya ya leo, leo yawe yamepita
Yaniepita na vilio, vilio vipishe nyota
Nyota njema ing’arao, ing’arao kunikita
Kunikita salamani, salamani nikadata.
MASWALI
a) Tambua nafsineni katika shairi hili (Alama 1)

b) Kwa nini nafsi neni inaomba subira na amani? (Alama 1)

c) Shairi hili ni la bahari gani kwa kuzingatia : (Alama 4)
(i) Mpangilio wa maneno
(ii) Mpangilio wa vina.
d) Kwa kutolea mifano eleza mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi. (Alama 4)

e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (Alama 4)

f) Kwa kutolea mifano, eleza jinsi uhuru wa kishairi ulivyotumiwa kutekeleza arudhi. (Alama 3)

g) Eleza umbo la shairi hili. (alama 3)

7. FASIHI SIMULIZI
(a)
i. Eleza mbinu tano za ukusanyaji wa data katika Nyanja. ( alama 5)
ii. Jadili changamoto zinazowakumba watafiti wanapokusanya data ya fasihi simulizi nyanjani. ( alama 10)
iii. Je, ,miviga ina hasara gani katika jamii? ( alama 5)
( b)

i. "Fasihi Andishi na Fasihi Simulizi hufanana" Tathmini ukweli wa kauli hii. (alama 5)
ii. Fafanua sifa za ushairi simulizi.(alama 5)
iii. Eleza sababu zozote tano zinazosababisha kubadilika kwa Fasihi Simulizi. (alama 5)
iv. Methali ni utanzu tegemezi. Fafanua (alama 5)

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOCHAPISHWA.

IDARA YA LUGHA
APRILI MWAKA 2020
KIDATO CHA NNE
102/2 – KISWAHILI – Karatasi ya 2
JINA__________________________________________ DAR_______
Sarufi Na Matumizi Ya Lugha (Alama 40)
a) Tolea sifa bainifu za sauti /r/. ( alama 2)

___________

b) Andika neno lenye muundo wa IKKIKIKI. ( alama 2)

__________

c) Eleza maana ya kiimbo. ( alama 1)

__________

d) Neno maiti liko katika ngeli ipi? ( alama 1)

__________

e) Eleza maana ya kiambishi. (alama 1)

__________

f) Tambua aina za maneno katika sentensi hii. ( alama 3)
Cha mlevi huliwa na mgema.

__________

g) Tambua kiima, kipozi na kitondo katika sentensi. (alama 3)
Aliwapikia wageni chakula kitamu.

__________

h) Tunga sentensi zenye vivumishi vinavyoleta dhana hizi: ( alama 4)
i. Nafasi katika orodha_______
ii. Bila kuchagua ___________
iii. Kumiliki _____________
iv. Kuashiria ukaribu _______
i) Tumia na ili kuibua dhana hizi: ( alama 4)
i. Kitenzi __________

ii. Kiunganishi ______
iii. Kihusishi ________
iv. Wakati _________
j) Changanua sentensi hii kwa njia ya matawi. ( alama 4)
Wasichana na wavulana walicheza sana ila walimu wao walikaa ofisini.

k) Nyambua vitenzi hivi vya silabi moja katika kauli ya kutendeka. (alama 2)
i. Fa _________
ii. Cha _______
l) Tambua aina za nomino katika sentensi hii.( alama 3)
Baraza la wazee lilibuniwa kuchunguza uhalifu katika eneo la Lanet. ____________
m) Vielezi vya wakati hutambulishwa kwa njia kadhaa. Taja njia zozote tatu. (alama 3)

____________

n) Bainisha viambishi kidhamira.( alama3)
Hatujampikia

o) Eleza maana ya msemo enda mbweu. ( alama 1) ___________

p) Andika katika usemi halisi. ( alama 3)
Waziri alisema kuwa ugonjwa wa Corona ni hatari. Aliwasihi raia kufuata sheria kama vile kukaa nyumbani , kunawa mikono na kutotangamana.

________________

ISIMU JAMII (ALAMA 10)
1. Eleza sababu tano zinazowafanya watu kuchanganya ndimi wakati wa mazungumzo. ( alama 5)

_________________

2. Tetea kauli kuwa Kiswahili ni lugha ya kimataifa. ( alama 5)

_________________

IDARA YA LUGHA
APRILI MWAKA 2020
KIDATO CHA NNE

102/3 – KISWAHILI – Karatasi ya 3
FASIHI

Maagizo:

g) Jibu maswali YOTE katika Karatasi hii.
h) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

SEHEMU A: TAMTHILIA YA KIGOGO ( PAULINE KEA)
1. Uongozi mbaya ni tatizo kubwa barani Afrika. Jadili hoja hii kwa kudhihirisha maovu yaliyotekelezwa na Majoka katika jimbo la Sagamoyo. ( alama 20)
SEHEMU B: RIWAYA YA CHOZI LA HERI (ASSUMPTA K. MATEI)
2. “wewe ni mfuata mvua”
a) Eleza muktadha wa dondoo.( alama 4)
b) Tambua umuhimu wa msemezwa. (alama 6)
c) Eleza matatizo yoyote manne yaliyomkumba msemezwa katika riwaya. ( alama 4)
d) Jadili suala la kifo katika riwaya. ( alama 6)

3.
a) Jadili dhana ya chozi kwa mujibu wa riwaya. ( alama 10)
b) Eleza jinsi mwandishi alivyofanikisha matumizi ya majazi. ( alama 10)

SEHEMU C: HADITHI FUPI YA TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE. (DUMU KAYANDA NA ALIFA CHOKOCHO)
Kidege (Robert W. Oduori
4. “ hanyee mwenye kasri hunyaa mwenye choo”
a) Eleza muktadha wa dondoo. ( alama 4)
b) Tambua mbinu ya lugha katika dondoo. ( alama 1)
c) Eleza sifa tano za msemaji. ( alama 5)
d) Jadili maudhui yafuatayo katika hadithi. ( alama 10)
i. Utabaka
ii. Dhuluma na unyanyasaji
5. Mwanamke bado ana kilio. Tetea kauli hii kwa kurejelea hadithi hizi: (alama 20)
i. Mwalimu Mstaafu
ii. Ndoto ya Mashaka
iii. Mame Bakari

6. SEHEMU D: USHAIRI
Mapenzi kitu ajabu, yakutia bumbuwazi

Yakufanya uwe bubu, kujibu huwa huwezi
Shubiri kwako zabibu, na vitamu huviwezi.

Wamkuta kaemewa, asemayo hayajuwi
Aumba akiumbuwa, aona maruwiruwi
Vigumu kumuopowa, na kwa ngisi kumvuwi.

Hukumbuka ya zamani, yote walofanyiana
Nyumbani barabarani, ayaona kama jana
Akili yake na nyani, aruka ingagongana.

Wangoja nyota ya jaha, kutwa wewe unahaha
Mawazo yako silaha, akukwaaye usaha
Usifanyiwe msaha, waugeuza karaha.

Kalelewa kaleleka, utani kwake ni mwiko
Njiani yeye na kaka, hapokei mauliko
Ghadhabu zake zap aka, hapendi maziko.

Na Hashil S. Hashil

a) Andika kichwa mwafaka cha shairi hili. (al 1)

b) Eleza umbo la shairi hili. (al 4)

c) Tambua tamathali za usemi alizozitumia msanii (al 4)

d) Taja na ufafanue uhuru wa mshairi. (al 2)

e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nadhari. (al 4)

f) Fafanua mambo matatu yanayohusishwa na mapenzi. (al 3)

g) Taja nafsi neni katika shairi hili. (al 1)

h) Taja toni ya mshairi huyu. (al 1)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

7.
a) Eleza maana ya: ( alama 4)
i. maigizo
ii. nyiso.
b) Je, nyiso zina umuhimu upi katika jamii? ( alama 5)
c) Fasihi simulizi na fasihi andishi zinafanana. Eleza. ( alama 6)
d) Fasihi simulizi inaelekea kufa. Tolea sababu zinazochangia hali hii. ( alama 5)

8. Dhima pekee ya hadithi ni kuelimisha. Jadili. ( alama 20)